# ‘Tega sikio ujifunze – Elimu ya Kawaida:EPISODE 8

## “Ni mnyama gani mwenye meno makali zaidi ulimwenguni, au katika shamba la wanyama”

**Makala : Leona Frommelt**
**Mwelekezi : Maja Dreyer**
**Tafsiri : Anne Thomas/Eric Ponda**

## Taarifa kwa mwelekezi

## Watu:

Mtangazaji
Jenny Msichana miaka 14
Jack Mvulana miaka 15
Mtaalam wa viumbe vya majini *(Sauti ya simu)*
Daktari wa meno

## Maeneo:

Shuleni / barabarani/
Nyumbani kwa Jack
Katika hospitali ya daktari wa meno

## Sauti:

Sauti za shuleni
Sauti za barabari
Sauti ya simu – ikipigwa, ikilia na ikiwekwa chini.
Kufungua kurasa za kitabu
Sauti za kutoboa kama zile za hospitali ya meno.

**OUTRIO (Mwanzo)**

**(mtangazaji)**
Hujambo na karibu katika vipindi vyetu vipya vya tega sikio ujifunze katika msururu wa elimu ya kawaida. Hii leo tutazungumzia meno hasa kumhusu Jack ambaye anaumwa na jino. Lakini uchungu huo haujamfanya yeye na rafiki yake Jenny kukosa kujifunza mengi kuhusu meno. Kwa mfano wanataka kujua ni mnyama gani mwenye meno makali zaidi ulimwenguni, pia wanataka kujua ni wanyama gani ambao huosha meno yao. Maswali hayo si rahisi lakini wachunguzi hao wanapata usaidzi kutoka kwa kwa daktari wa meno wa Jack.

**Scen 1 :*Jenny na Jack wamekutana barabarani baada ya shule.***

***(kwa mbali – watoto wakicheza na sauti za barabara).***

**Jenny:**Hujambo Jack?

**Jack:**Oooh!

**Jenny:** Una nini wewe?

**Jack :***(Akilalamika)* Ninaumwa na jino.

**Jenny:**Pole sana. Labda jino lako lina shimo.

**Jack:** Hata mimi nafikiria hivyo.!

**Jenny:**Basi ni muhimu uende ukamuone daktari wa meno

**Jack:** Nani? Siendi kumuona daktari yeyote. Nitangojea hadi pale uchungu utakapoisha wenyewe.

**Jenny**: Hautaisha!. Ukimuona daktari akutibu ndiyo uchungu huo utaisha haraka.

**Jack:**Lakini mimi sipendi daktari. Nasikia uoga nikifikiria kudungwa sindano.

**Jenny:** Upuzi. Sindano haiumizi chochote. Ama unataka nikungoe jino hilo mwenyewe?.

**Jack:** Haiwezekani!!!. Mimi nakujua wewe unaweza kulingo'a, siutani!.

**Jenny:** Nionyeshe ni jino lipi?

**Jack:** Moja ya haya ya hapa mbele. Upande wa juu!.

**Jenny:** Wajua, Jack, ni aibu wewe hukuzaliwa mbuzi.

**Jack:** Mbuzi? Unasema nini wewe?

**Jenny:**Eee Mbuzi. Kama ungekuwa mbuzi meno yako ya mbele hayangekuuma.

**Jack:** Kwa nini?

**Jenny:**Kwa sababu mbuzi hana meno ya juu na badala yake ana ki-ufizi tu upande wa juu. Mbuzi wana meno ya chini tu.

**Jack:** Kwa nini mbuzi ana -kiufizi tu?

**Jenny:** Kwa sababu yeye ni wa jamii ya wanyama wanaokula majani. Wao hula mchana mzima na kisha jioni lazima wateuke na kusage majani, nyasi na vijiti wanavyokula. Kwa hivyo kifizi hicho huwasaidia.

**Jack:** Kama ningekuwa mbuzi basi, kifizi changu kingeuma sana.

**Jenny:** Wacha kujihurumia kiasi hicho Jack. We ni mwanamme.

**Jack:**Wajua Jenny, niheri kama ningekuwa na meno ya papa!.

**Jenny:** Kwa nini? Kwa sababu ni makali na ni hatari unaweza kumuuma mtu nayo?

**Jack:** Si hivyo, Kuna sababu nyingine. Hebu fikiria. Na unapofikiria nataka niende nyumbani niweke kitu mdomoni ili jino hili liache kuuma.

**Jenny:** Sawa.Nitakuona baadaye. Lakini kwa sasa nitakifiria kuhusu siri ya meno ya papa. Kumbuka kutafuta ni mnyama gani mwenye meno hatari zaidi duniani.

**Jack:** Sawa. Nitajaribu!.

**Muziki….**

**------------------------------------------------------------------------------------------------------------**

***Scene 2 (Nyumbani kwa Jack)***

**------------------------------------------------------------------------------------------------------------**

**Jenny:** Jack, Vipi?

**Jack:***(Akinung'unika)* Sijasikia vizuri bado. Je unajua ni kwanini ningependelea kuwa na meno ya papa katika hali hii niliyo nayo?

**Jenny:**Nafikiria nimejua. Nina rafiki mmoja anajuana na mtaalamu wa maswala ya viumbe wa majini ambaye nilimuuliza.

**Jack:**Na akakwambia nini?

**Jenny:**Naam , ilikuwa hivi …

***Muziki kwa chini kwa chini kwenye onyesho la kukumbuka.***

*(Simu inalia --)*

**Mtaalamu:**Ni Peter Didamwe anayeongea.

**Jenny:** Hello, Mimi naitwa Jenny. Nataraji sijakusumbua…. Nilipata nambari yako ya simu kutoka kwa rafiki yangu …

**Mtaalamu:** Hello Jenny nikusaidia vipi.?

**Jenny:**Ningependa kujua ni nini cha mno katika meno ya papa, nini spesheli katika meno hayo?.

**Mtaalamu:**Swali nzuri. Je unajua meno ya papa yanaitwaje?

**Jenny:** Sina hata ufahamu!

**Mtaalamu:**Yanaitwa meno ya mzinga wa kuzunguka . Unajua ni kwa nini?.

**Jenny:**Hata habari sina!

**Mtaalamu:** Kwa sababu papa ana safu kadhaa ya meno. Likivunjika moja, jingine linatokezea katika muda wa masaa machache tu!. Papa wengine hutumia hata meno mia moja kwa mwaka. Ufizi wa papa ni kama mzinga uliotiwa meno ya kuzunguka na ndio sabau unaitwa mzinga.

**Jenny:** Ala, hiyo inamfaa. Pia sisi kama tungekuwa na meno ya mzinga wa kuzunguka, ingekuwa rahisi, ukiumwa na jino na ling'oke mara moja jingine jipya linamea.

**Mtaalamu:** Kabisa!

**Jenny:** Si hivyo engekuwa bora zaidi!. Hatungefikiria meno yetu. Sasa nimefahamu kwa nini Jack angetaka kuwa papa.

**Mtaalamu:** Ahh? Jack ni nani?

**Jenny:** Usijali!. Lakini asante sana kwa habari hizo muhimu.

**Mtaalamu:** Nafurahi kwamba umesaidika!. Uwe mwangalifu na msalimie huyo Jack.

***(Mwisho wa mazungumzo ua simu) Musiki unaisha***

**Jack:** Ni kweli alinisalimia?

**Jenny:** Kweli!, Lakini Jack wajua wewe si papa na unajua hauna meno mengine kuchukua nafasi ya lile linalouma. Kwa hivyo lazima umuone daktari wa meno.

**Jack:** Nitaenda. Nitaenda basi!. Nilikuwa nataka kukwambia ni mnyama gani mwenye meno hatari zaidi duniani.

**Jenny**: Nikusikiliza!

**Jack:** Bila shaka ni ndovu. Unajua mikonga yake inaweza kua mirefu kiasi gani?

**Jenny:** Sina habari. Mita moja labda?

**Jack:** Kweli. Hata mita tatu unusu!. Huo ni urefu wa gari na pia mikonga inaweza kuwa mizito sana!. Inaweza kuwa na uzito wa kilo mia moja. Fikiria kama ungeambiwa ubebe mmoja?.

**Jenny:** Nitakataa, Asante!

**Jack:** Situ kwamba ndovu wanamikonga mirefu bali pia wana meno mazito kama mawe.

**Jenny:** Ni vizuri una meno madogo. Lau sivyo yangekuuma zaidi.

**Jack:** Ni kweli kabisa!. Lakini wajua kuna mnyama mwingine ambaye ana meno madogo kuliko yale ya ndovu lakini hatari zaidi. Hebu fikiria ni mnyama gani ninayemzumguzia.

**Jenny:** Sawa!. Nikishinda uahidi kuwa utaenda kumuona daktari mara moja. Ahidi?

**Jack:** Ninaahidi. Lakini najua hutajua!.

Jenny: Basi tuonane baadaye!

**Muziki…...**

**-----------------------------------------------------------------------------------------------------------**

***baada ya shule tena***

**-----------------------------------------------------------------------------------------------------------**

***Sauti za watoto wakicheza kwa mbali na sauti za barabara kama pale kwanza.***

**Jack:** Hujambo Jenny!

**Jenny:** Jack, wajisikiaje? Meno yako yako je?

**Jack:** Um, bado sijasikia vizuri. Lakini nieleze kuhusu uchunguzi wako. Umejua ni mnyama gani mwenye meno hatari zaidi? Najua bado hujafanikiwa.

**Jenny**: Mwanzoni nilifikiria unazungumzia samba.

**Jack:** Kwa nini?

**Jenny:** Kwa sababu simba ana meno makali. Ni lazima yawe makali kwa sababu wao hula nyama. Wana meno ya mbele ambayo yameundwa spesheli kukamata windo lao na kisha kulikatakata vipande.

**Jack:** Ni kweli. Siwezi taka kukutana na simba mwenye hasira katika usiku wa kiza. Lakini nafikiria kuna mnyama mwingine ambaye ana meno hatari zaidi, kwa hivyo hujashinda shindano hili.

**Jenny:** Ngoja nafikiri, nimejua unaamanisha mnyama gani.

**Jack:** Ni yupi basi?

**Jenny:** Nyoka wenye meno ya sumu. Kama vile swila na aina nyingine ya nyoka. Meno yao ni kama sindano hatari. Sumu inayotoka vinywani mwao hupitia ndani ya jino wanapouma kitu. Hali hii inafanya aliyeshambuliwa kulemewa haraka au hata kufariki pao hapo. Je nimeshinda?.

**Jack:** Ndio, nilifikiria kuwa hutajua?

**Jenny:** Nilimuuliza mwalimu wetu wa somo la bayolojia. Unajua kama ungekuwa nyoka wa sumu, jino lako halingekuwa likikuuma!.

**Jack:** Kwa nini?

**Jenny:** Kwa sababu meno ya nyoka wa sumu hutoka tu wakati wanatoa sumu na kisha kumezwa tena. Nyoka hawana meno ya kula windo lao, au kulikatakata vipande. Lakini wanaweza pia kupanua mdomo ili kuweza kumudu windo kubwa kuliko midomo yao.

**Jack:** Lo! Sitaki kufikiria jambo kama hilo!

**Jenny:** Lakini ni jambo la kufurahisha!. Nyoka humeza mnyama mzima na kisha kutumia misuli ya meno yake kumlainisha ili aingie katika tumbo lake ambako atasagwa. Hali hiyo inaweza kuchukua muda wa siku kadhaa!

**Jack:** Hii ndiyo sababu nyoka hawaonekani kula kila wakati…….

**Jenny:** Kabisa! Na sasa Jack tunaenda sote kwa daktari wa meno.

**Jack:** Tunaenda? Kwani tunaandamana?

**Jenny:** Si ndiyo, nitakushika mkono. Haya twende!.

**Muziki……**

---

***Jenny na Jack wakiwa kwa daktari wa meno***

**---------------------------------------------------------------------------------------------------------**

**Chini kwa chini…Sauti ya kutoboa ikielekea kuisha**

**Jenny:** Waona haikuwa baya vile ulivyofikira!!!

**Jack:** Ni kweli! nimefurahi hakulitoa jino hilo.

**Daktari wa kike:** Waona Jack!, kama ungekuja mapema, hungesikia uchungu kiasi hicho.

**Jenny:** Ni lazima uwe unaosha meno yako vizuri kila wakati.

**Daktari:** Rafiki yako amesema kweli

**Jack:** Daktari, je wanyama pia huosha meno yao?

**Daktari:** Wengi wao hawaoshi. Kwa mfano wanyama kama vile panya--- hutumia meno yao na kisha mengine kumea mara moja.

**Jack:** Na wanyama wengine hufanyaje?

**Daktari:** wanyama kama vile mamba wanatumia ndege ambao huingia vinywani mwao na kuosha meno. Lakini wanyama wanaowinda huosha meno yao wanapokula. Wao hula mifupa na manyoya ambayo huosha meno yao. Ikiwa wanyama hawa wangekula nyama tu, basi meno yao yangeng'oka yote!.

**Jack:** Mimi sioni nikila chochote hadi kufikia mifupa. Ni heri ninywe supu wakati huu!.

**Jenny:** Sawa twende nyumbani nikakutengezee supu na baada ya hapo unaweza kufanya kama tumbili!.

**Jack:** Tumbili?

**Jenny:** Tumbili huosha meno yake kwa vijiti lakini badala yake utatumia mswaki.

**Jack:** Utakavyosema Bi Daktari Jenny!.

**Jenny na Jack:** Kwa kheri Daktari!

**Daktari** *(akicheka )* Kwa herini nyote!

**Muziki – mwisho…….**

**<u>mtangazaji</u>**

Lililo nzuri huisha kwa uzuri. Hivi karibuni Jack ataweza kuuma vitu na hakutakuwa na haja yake kufanya mashindano ya elimu ya kawaida kati yake na Jenny. Ni hayo kwa leo katika msururu wetu wa vipindi vya elimu ya kawaida . Mchezo huu

umeandikwa na na Leona Fennet. Unaweza kusikiliza kipindi hiki tena na vingine kupitia mtandao wetu http://www.dw.de/kiswahili. Asante kwa kusikiliza na usisahau kuwa nasi tena wakati mwingine. Kwaheri.